# OFISI YA RAIS - TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

SHULE YA SEKONDARI BULYAGA,
S.L.P 641,
**TUKUYU.**
Tarehe 07-12-2020

Kumb. Na.BSS / S3494 / KDI-2021 / VOLXV /........

Mwanafunzi.......................................................
S.L.P................................................................
**TUKUYU.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BULYAGA JANUARY- 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukujulisha kuwa miongoni mwa watanzania wengi umebahatika kuchaguliwa kujiunga **kidato cha kwanza (I) mwaka 2021** katika Shule ya Sekondari Bulyaga. Shule hii ipo umbali kilometa mbili (02) Kaskazini Mashariki kutoka makao makuu ya halmshauri ya wilaya ya Rungwe.

Muhula wa masomo kwa mwaka -2021 utaanza tarehe **11-01-2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **tarehe 11-01-2021. Siku ya Jumatatu, saa 01:00 asubuhi**; Ukiwa na mahitaji yote ya muhimu uliyoagizwa na mwisho wa kuripoti ni **tarehe 18-01-2021.**

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare za shule hii na mahitaji mengine muhimu:**

**(a) Wavulana**

(i) Suruali mbili (02); nadhifu zenye marinda mawili na zenye mkunjo chini ‘turn-up’, moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya kijani jeshi. (vitambaa vimeambatanishwa).

(ii) Shati mbili (02); ziwe nyeupe zikiwa na mikono mifupi. Tai mbili; zifanane na kitambaa cha suruali.

(iii) Viatu vya ngozi jozi mbili (02) vyenye kamba, viwe vyeusi vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi pea mbili (02).

(iv) Sweta moja (01) liwe rangi ya kijani jeshi, uzi wa sweta hilo umeambatanishwa

(v) Sare za michezo mbili (02);”Tracksuit”rangi bluu bahari yenye ufito mweupe, jezi nyeusi na viatu vya michezo.

(vi) Vifaa vya kujifunzia, seti ya mkebe moja, ‘mathematical table’ moja, rula sentimeta 30 na kamusi ya kiingereza na bunda moja la karatasi(ream paper) kwa ajili ya mitihani ya kila wiki(weekly test).

(vii) Mkoba nadhifu wa kubebea daftari kumi (10 - counter book-quire 3) pamoja na vitabu.

(vii) Vifaa vya usafi wa mazingira ya shul:- ufagio wa chelewa mmoja (01), mopper na ndoo(20Ltr) moja.

**(b) Wasichana**

(i) Sketi mbili (02); zivuke chini ya goti kwa kiasi cha zaidi ya sentimeta 30; moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya kijani jeshi (vitambaa vimeambatanishwa)

(ii) Blauzi mbili (02); ziwe nyeupe zikiwa na mikono mifupi. Tai mbili zifanane na kitambaa cha sketi.

(iii) Viatu vya ngozi jozi mbili (02) vyenye kamba; viwe vyeusi vyenye visigino vifupi na soski nyeupe pea mbili.

(iv)Sweta moja (01); liwe rangi ya kijani jeshi, uzi wa sweta hilo umeambatanishwa.

(v)Sare za michezo mbili (02);’’Tracksuit” rangi bluu bahari yenye ufito mweupe na jezi nyeusi na viatu vya michezo.

(vi) Vifaa vya kujifunzia; seti ya mkebe moja, “mathematical table’’ moja, rula sentimeta 30’ kamusi ya kiingereza na bunda moja la karatasi(ream paper) kwa ajili ya mitihani ya kila wiki (weekly test).

(vii) Mkoba nadhifu wa kubebea daftari kumi (10 - counter book- quire 3) pamoja na vitabu.

(viii) Vifaa vya usafi wa mazingira ya shule; ufagio wa chelewa mmoja (01), “soft bloom” moja, na ndoo moja(20Ltr).

**2.2 Chakula cha mchana kwa mwanafunzi wa kutwa ni jukumu la mzazi/mlezi wake;** hivyo basi ukiwa katika shule hii, uongozi wa shule utatoa nafasi kwa mzazi/mlezi wako ili akutane na kamati ya wazazi inayoratibu shughuli nzima ya upatikanaji wa chakula hapa shuleni. Mzazi/mlezi wako afike tarehe **22-12-2020,** siku ya **Jumanne**, **saa 03:00 asubuhi** bila kukosa ili akutane na uongozi wa shule na kamati ya wazazi/walezi kwa ufafanuzi zaidi.

## 3:0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

3:1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi, Teknolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya **Rais – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo; ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(Preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu yakuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, vifaa na mazingira yote ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote uwapo shuleni na nje ya shule, na;
i) Kutunza mali zote za umma.

## 3:2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:

a) Wizi;
b) Uasherati na ushoga;
c) Ubakaji;
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya;kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k;
e) Kupigana au kupiga;
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma;
g) Kudharau bendera ya Taifa;
h) Kuoa au kuolewa;
i) Kuwa mjamzito au kupata mimba;
j) Kutoa mimba;
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu;
l) Kukataa adhabu kwa makusudi; na
m) Kuwa na simu ya mkononi.

## 4:0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA NA MWANAFUNZI KATIKA SHULE HII.

4:1. "Medical examination form" ambayo itajazwa na Mgamga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

4:2. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai, na

4:3. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5:0. Tafadhari soma kwa makini yote, maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA BULYAGA SEKONDARI**
**"ELIMU NI MWANGA NA MSINGI WA MAISHA"**

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
# SHULE YA SEKONDARI BULYAGA
# S.L.P 641, TUKUYU

**<u>FOMU YA MKATABA WA UWAJIBIKAJI NA UTII</u>**

**(ijazwe na kurejeshwa shuleni)**

**SEHEMU A: MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi..............................................................nimesoma vizuri na kwa umakini kanuni na sheria za shule na kuzielewa vema. Ninaahidi kuzifuata na kuzitii bila shuruti sheria na kanuni zote za shule katika kipindi chote cha uanafunzi wangu ndani ya shule na nje ya shule. Vilevile ninaahidi kutekeleza wajibu wangu wote nyumbani na shuleni. Nikikiuka na kuvunja kanuni na sheria za shule, nipo tayari kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

Majina kamili ya mwanafunzi.............................................................................................................
Sahihi................................................Tarehe............................................................................

**SEHEMU B:MZAZI / MLEZI (namba ya simu..........................................................................)**

Mimi ..................................................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi.................................................................................................. nakubaliana na masharti, sheria na Kanuni za shule hii , na kwamba ninaahidi kumlea mtoto wangu katika misingi na maadili stahiki na nitatoa ushirikiano kwa walimu na uongozi katika malezi, na mahitaji yote muhimu ya shule. Nitafika shuleni pale nitakapoitwa na uongozi wa shule na vilevile kwa nia ya kufuatilia maendeleo ya mtoto wangu katika tabia na taaluma kwa wakati wote atakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

Jina la mzazi/mlezi...........................................................................................................
Kata ya..........................................................................................................................
Namba ya simu ya mtendaji kata.......................................................................................
Kijiji cha........................................................................................................................
Sahihi......................................................... tarehe...............................................................

**SEHEMU C: MKUU WA SHULE**

Uongozi wa shule ya sekondari Bulyaga unamtakia mwanafunzi masomo mema na ushirikiano mwema katika kukiinjika chungu hiki cha **Taaluma** katika mafiga matatu ya ushirikiano, ambayo ni mwanafunzi, mzazi/mlezi na walimu/uongozi wa shule. Ili kupata chakula bora maana yake mafanikio katika **Taaluma.**

**KWA PAMOJA TUNAWEZA**

**.........................................................**

**MWAKIPUBA, F. A**

**(MKUU WA SHULE)**